

MKATABA WA UPANGAJI

Mkataba huu wa umefanyika leo tarehe...Mwezi...2021

KATI YA

GASPER DANIEL SUMBALI wa wa sanduku la Posta 4422 Dodoma (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "Mpangishaji") kwa upande mmoja.

NA

LAND NETWORK LIMITED wa wa sanduku la Posta 3118 Dodoma (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "Mpangaji") kwa upande mwingine.

Mkataba huu umeshuudia kama ifuatavyo:-

1. Kwamba, mpangishaji anampangisha mpangaji vyumba kwenye Kiwanja No 3 Kitalu "N" Uhindini Dodoma Manispaa.
2. Mkataba huu ni wa kipindi cha Miaka Mitatu (3) ambao unaaanza tarehe 01/08/2021 hadi tarehe 31/07/2024.
3. Kwamba, kodi ya pango ya vyumba hivyo vitatu (3) ni shilingi Milioni Moja (Tshs 1,000,000/=) kwa mwezi kodi ambayo imelipwa kwa mkupuo kiasi cha Shilingi Milioni Themathini na Sita (Tshs 36,000,000/=).
4. Kwamba, Mpangaji ameweka kiasi hicho cha fedha kwenye Akaunti ya Benki ya NMB A/C NO. 50503300062 yenye Jina la BAHU COMPUTERS EXPRESS.
5. Kwamba, mara baada ya kumalizika kwa kodi iliyoanishwa katika kipengele namba 3 Mpangishaji na mpangaji wanaweza kufanya mazungumzo juu ya ongezeko la kodi ya vyumba tajwa au la.
6. Kwamba, Mpangaji anapaswa kulipa kodi ndani ya makubaliano yaliyopangwa, iwapo hatafanya hivyo atalipa 10% ya tozo ya kodi ya mwezi/ miezi aliyotumia kwa kuwa Jengo lipo kibiashara.

MKATABA HIJU UNASIIHUUDIWA NA MPANGAJI KAMA IFUATAVYO:-

- (a) Kwamba, Mpangaji anaahidi kulipa kodi kama ambavyo wamekubaliana na mpangishaji
- (b) Kwamba, Mpangaji hataruhusiwa kufanya marekebisho yoyote kwenye eneo hilo bila ruhusa ya mpangishaji (mwenye eneo).


- (c) Kwamba, endapo mpangaji ataamua kuhama katika Nyumba husika basi kwa kumpa taarifa mpangaji ataoa vifaa vile vyenye uwezekano wa kutoka bila kuadhiri muonekano wa vyumba alivyopanga. Mfano milango na madirisha.
- (d) Kwamba, mpangaji atafanya matengenezo madogo madogo katika vyumba alivyopangishwa katika hali itakayoendana na kazi zake za kiofisi. Matengenezo hayo yatakuwa ni pamoja na kugawa vyumba vidogo vidogo vya muda (temporary partition) na kuweka gypsum na vifaa vingine vya kiofisi katika nyumba tajwa bila kuathiri nyumba husika kadri anavyoona inafaa kwa kushauriana na mpangishaji kwa gharama zake bila ya kudai malipo kutoka kwa mpangishaji,
- (e) Kwamba, endapo kutatokea janga la kibinadamu kama vile moto, radi, maftiriko nk, yakafanya vyumba alivyopanga kuwa vibovu, makato ya fedha zilizokwisha kulipwa yatasimamishwa mpaka pale nyumba hiyo itakapo tengenezwa upya, na kama matengenezo hayo hayatafanyika ndani ya miezi kumi na mbili (12) mpangishaji atalazimika kumrudishia mpangaji kiasi kilichobaki kulingana na miezi iliyokuwa aijaisha kwa nujibu wa mkataba huu na mkataba huu utasitishwa mara moja.
- (f) Kwamba, Mpangaji au nmpangishaji hataruhusiwa kuweka mpangaji mwingine ndani ya kipindi hiki cha mkataba.
- (g) Kwamba, mpangaji atatakiwa kulipa gharama za umeme jinsi atakavyotumia kwa kipindi chote cha mkataba wa Miaka mitatu (3).
- (h) Kwamba, mpangaji atatakiwa kutumia eneo hilo kwa ajili ya biashara tu na si vinginevyo.
- (i) Kwamba, Mpangaji au Mpangishaji atatakiwa kutoa taarifa mwezi mmoja kimandishi kabla ya Mkataba huu wa Miaka mitatu (3) kwisha kama ataendelea na mkataba au la.
- (j) Kwamba, mpangaji atatakiwa kutoa kodi ya pango iliyo kamili yaani kodi ya muda husika aliopanga na sio kutoa kidogokidogo.

MWENYENYUMBA NAYE ANAKUBALI IFUATAVYO.-

- (k) Kuhakikisha kwamba taarifa zote ambazo anatakiwa kumpa mpangaji zinamfikia kwa njia ya anwani yake na mkono kwa mkono.
- (l) Kulipa kodi ya Jengo kuepusha usumbufu kwa mpangaji.
- (m) Endapo Mwenyenyumba atapanga kufanya marekebisho makubwa katika Nyumba hiyo ambayo yanaweza kuikwaza biashara ya mpangaji, atatoa taarifa mapema kwa njia ya majadiliano na mpangaji.

KWA UTHIBITISHO, wahusika wameweka sahihi katika mkataba huu kwa namna na tarehe kama inavyoonekana hapa chini.

UMESAINIWA NA KUWASILISHWA kwangu na
GASPER DANIEL SUMBALI ambaye
namfahamu binafsi/ametambulishwa kwangu na
ambaye namfahamu binafsi mbele yangu leo
tarehe . . . 01mwezi . . 082021.




MBELE YANGU:

SAHIHI



JINA: HUSSEIN ASSERI MANDARI
ANUANI YA POSTA : S.L.P 3118
DODOMA

UMESAINIWA NA KUWASILISHWA kwangu na
LAND NETWORK LIMITED ambaye
namfahamu binafsi/ametambulishwa kwangu na
ambaye namfahamu binafsi mbele yangu leo
tarehe . . 01 . . .mwezi . . 08 . . .2021.



MBELE YANGU:

SAHIHI



JINA: HUSSEIN ASSERI MANDARI
ANUANI YA POSTA : S.L.P. 3118
DODOMA